Rasimu ya Pili ya KATIBA Inasemaje ?

Chapisho la Lugha Nyepesi

Rasimu ya Pili ya KATIBA Inasemaje ?

Chapisho la Lugha Nyepesi

Kimeandikwa na :

1. National Council for NGOs (NACONGO)
2. Legal and Human Rights Centre (LHRC)
3. Tanzania Gender Network Programme (TGNP)
4. Muungano wa Vyama vya Wakulima Tanzania (MVIWATA)
5. Trade Union Congress of Tanzania (TUCTA)
6. Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA)
7. Shirikisho la Vyama vya Walemavu Tanzania (SHIVYAWATA)
8. Information Centre for Disabilities (ICD)
9. Child Development Forum (CDF)
10. Jukwaa La Katiba Tanzania (JUKATA)
11. Tanzania Network of Legal Aid Providers (TANLAP)
12. Policy Forum
13. Tanzania Media Women Association (TAMWA)
14. Haki-ardhi
15. Tanzania Youth Coalition (TYC)
16. Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)

Kimehaririwa na :

Dr. Helen Kijo-Bisimba
Harold Sungusia
Anna Henga
Rose Lugakingira
Alex Modest

Mchora katuni : Nathan Mpangala

Kimechapishwa na Policy Forum

Teleo la Kwanza- februari, 2014

ISBN : 978-9987-708-12-3

Kimesanifiwa na kupigwa chapa na :
C I GROUP LTD
SLP 70792
Dar es Salaam, Tanzania

YALIYOMO

UTANGULIZI iii
SURA YA KWANZA 1
Masuala chanya katika Rasimu ya Katiba 1
DHAMIRAYA KWANZA 1
MAMBO YA JUMLA 1
Lugha 1
Alama na Siku za Taifa 2
Tunu za Taifa 2
DHAMIRA YA PILI 3
HAKI ZA BINADAMU 3
Haki za Makundi 4
Haki za Wanawake 4
Haki za Wazee 5
DHAMIRA YA TATU 6
UTAWALA NA SERIKALI 6
DHAMIRA YA NNE 6
BUNGE 6
DHAMIRA YA TANO 6
MAHAKAMA 6
UTUMISHI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO 7
DHAMIRA YA SITA 8
UCHAGUZI NA VYAMA VYA SIASA 8
DHAMIRA YA SABA 8
MUUNDO WA JAMHURI YA MUUNGANO 8
DHAMIRA YA NANE 8
TAASISI ZA UWAJIBIKAJI 8
Tume ya Mahusiano na Uratibu wa Serikali (Ibara ya 109) 8
Tume Huru ya Uchaguzi 9
Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji 9
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 9
HITIMISHO 10

UTANGULIZI

Tanzania ipo katika mchakato wa Katiba tangu mwanzoni mwa mwaka 2011. Hatua kadhaa zimeshapitiwa katika mchakato huu muhimu kwa Taifa letu kama ifuatavyo; Kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011, kuundwa kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa mujibu wa sheria, Tume kuanza kazi kwa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu katiba mpya, Tume kutoa Rasimu ya kwanza ya Katiba na hatimaye Rasimu ya pili ya Katiba.

Rasimu ya pili ya Katiba ilikabidhiwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano mnamo tarehe 30/12/2013 kwa mujibu wa Sheria. Rais alichapisha rasimu hiyo kwenye Gazeti la Serikali na hatimaye kuiwasilisha kwenye Bunge Maalum la Katiba kabla ya wananchi kuipigia kura kupitia Kura ya Maoni.

Hivyo, kijitabu hiki kinaielezea Rasimu hiyo ya pili ya Katiba kwa lugha nyepesi. Kijitabu hiki kimeandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ili kuwawezesha watanzania wote kuisoma na kuielewa kwa urahisi Rasimu ya pili ya Katiba ili waweze kufuatilia mchakato wa mabadiliko ya Katiba hususani wakati Bunge Maalum la Katiba litakapoanza kuijadili rasimu hii.

Kijitabu hiki kimegawanyika katika sura 8 ambazo ni dhamira kuu za rasimu (themes) kama ifuatavyo;

i Mambo ya jumla
ii Haki za Binadamu
iii Utawala na Serikali
iv Bunge
v Mahakama
vi Muungano
vii Vyombo vya Kikatiba na Taasisi za uwajibikaji
viii Uchaguzi na Vyama vya Siasa

Ni imani yetu kuwa kijitabu hiki kitakuwa cha manufaa katika mchakato huu adhimu wa Katiba.

SURA YA KWANZA

Masuala chanya katika Rasimu ya Katiba

Kwa ujumla rasimu ya pili imeboresha mambo machache kutoka rasimu ya kwanza na pia imeongeza ambayo hayakuwepo. Vilevile kwa kuangalia rasimu hii inaonyesha jinsi gani Tume ya Mabadiliko ya Katiba imechukua mapendekezo mengi yaliyotolewa na wananchi kupitia mabaraza ya katiba ya wilaya na asasi mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye sheria.

Rasimu ya kwanza ilikuwa na Ibara 240 ambapo hii ya Pili ina ibara 271. Kuna vifungu ambavyo vimebadilika na ambavyo vimeongezeka kama itakavyooneshwa katika sura za kijitabu hiki.

Baadhi ya masuala chanya ni kama yafuatavyo;

i Kuhusu tume huru ya uchaguzi: Ibara ya 191 imetoa fursa kwa asasi za kiraia zisizokuwa za kiserikali kupendekeza majina ya watu wanaoweza kuteuliwa kuwa mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wa Tume huru ya uchaguzi

ii Kutoa tafsiri ya makundi madogo. Ibara ya 46.

iii Kufafanua zaidi Haki za wanawake kupata fursa sawa za ajira na pia kuondoa utata kuhusu haki ya wanawake za kiafya. Ibara Ibara ya 47.

iv Kuongeza mikataba ya Kikanda katika mikataba ya kimataifa. Ibara ya 53. Mikataba ya kikanda ni kama vile Mkataba wa Afrika wa haki za Wanawake, Mkataba wa Jinsia na Maendeleo wa nchi za SADC na Mkataba wa Afrika wa haki na ustawi wa mtoto.

v Kuendelea kuwepo kwa asilimia 50 kwa 50 ya wabunge wanawake na wanaume.

vi Uwepo wa wananchi kumwajibisha mbunge wao, na kadhalika.

DHAMIRA YA KWANZA: MAMBO YA JUMLA

Lugha

Lugha ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano imetamkwa kuwa ni Kiswahili na itatumika katika mawasiliano rasmi ya kitaifa na kiserikali, Ibara ya 4(1). Pia Rasimu imeeleza kuwa Serikali itaweka mazingira yanayowezesha

kuwepo kwa mawasiliano ya lugha mbadala zikiwemo lugha za alama kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum, Ibara ya 4(3). Rasimu ya katiba ibara 4(2) pia imetaja Kiingereza kama lugha inayoweza kutumika na lugha zinginezo iwapo zitahitajika.

Alama na Siku za Taifa

Katika ibara ya 3 ya Rasimu imeelezwa kuwa alama za Taifa ni a) Bendera ya Taifa, b) Wimbo wa Taifa na c) Nembo ya Taifa. Pia sikukuu za kitaifa zimetajwa kuwa ni; a) Siku ya Uhuru wa Tanganyika tarehe 9 Desemba, b) siku ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 12 Januari, c) Siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili na siku nyingine zitakazoainishwa na sheria za nchi. Sikukuu za kitaifa zitakuwa ni siku za mapumziko kwa mujibu wa ibara hii 3(3). Masuala yote haya yamebakia kama yalivyokuwa katika rasimu ya kwanza ya Katiba.

Tunu za Taifa

Rasimu imeeleza katika Ibara ya 5 kuwa Tunu za Taifa ni Utu, Uzalendo, Uadilifu, Umoja, Uwazi, Uwajibikaji na Lugha ya Taifa. Hapa tunu tunaweza kuzielezea kuwa ni uthamani wa Watanzania yaani yale mambo ambayo yanafanya uonekano wa nchi na watu wake katika uthamani na heshima

yao. Tunu hizi pia hazijabadilika, ziko kama zilivyokuwa kwenye rasimu ya kwanza ya Katiba.

DHAMIRA YA PILI: HAKI ZA BINADAMU

Haki za Binadamu zimeorodheshwa katika Sura ya Nne ya Rasimu ya pili zikiwa na sehemu kuu mbili yaani a)haki za binadamu (sura ya 23 had 48) na b) wajibu wa raia na mamlaka za Nchi na mipaka ya haki za binadamu (Ibara ya 49 hadi 55).

Haki za binadamu zilizoanishwa baadhi ni haki ambazo zilikuwepo tayari katika katiba ya mwaka 1977 inayotumika sasa. Hata hivyo kuna haki ambazo hazikuwepo kabisa katika katiba ya sasa ambazo zimeongezewa baada ya mapendekezo ya wananchi.

Haki hizo ni pamoja na haki za makundi ambazo zimeainishwa kuanzia Ibara ya 43 hadi ya 48 ya Rasimu ya Katiba. Haki hizo ni pamoja na haki ya mtoto, haki na wajibu wa vijana, haki za watu wenye ulemavu, haki za makundi madogo katika jamii, haki za wanawake na haki za wazee.

Haki hizi hazijafanyiwa maboresho yoyote ya kina kutoka katika rasimu ya kwanza ukiacha nyongeza katika ibara ya 46 ambayo kwenye rasimu ya kwanza ilikuwa ni ibara ya 45 inayohusu haki za makundi madogo katika jamii ambayo imefafanuliwa zaidi. Nyongeza hii ni kifungu kidogo cha 3 katika ibara hii ya 46 ambacho kinatoa tafsiri ya 'makundi madogo' yaani "jamii za watu wanaoishi kwa kutegemea uoto wa asili na mazingira yanayowazunguka kwa ajili ya chakula, malazi na mahitaji mengine ya maisha". Tafsiri hii itasaidia kuelewa maana ya makundi madogo ili wanapodai haki zao wajulikane walengwa hasa ni nani. Vilevile katika ibara ya 25 iliyokuwa ibara ya 24 katika rasimu ya kwanza, katika ibara ndogo ya 5 neno 'ulemavu' limeongezwa kwenye tafsiri ya neno 'kubagua'.

Angalizo; haki ya kuishi kwa mujibu wa Ibara ya 24 ambayo kwenye Rasimu ya Kwanza ilikuwa Ibara ya 23 bado imeminywa kwani imewekwa kwa mujibu wa sheria. Hii inahalalisha kutungwa kwa sheria inayoweza kuondoa uhai kama ilivyo sheria ya sasa inayoruhusu ya adhabu ya kifo.



Haki za Makundi

Haki za Mtoto - Ibara ya 43 ambayo ilikuwa ibara ya 42 katika rasimu ya kwanza, zimeboreshwa zaidi kwa kuongezwa kifungu kidogo cha 3 kinachotoa wajibu kwa mzazi, mlezi, jamii na mamlaka za nchi kuhakikisha mtoto analelewa katika maadili stahiki kwa umri wake.

Haki za Wanawake

Katika Ibara ya 47 ambayo mwanzoni ilikuwa Ibara ya 46, Haki za wanawake zimeendelea kuwepo. Haki hizo zimeboreshwa kidogo hususani ibara ndogo ya (g) ambayo kwenye mabaraza ya katiba ililalamikiwa sana kuwa ilikuwa imewekwa kimtego. Ilikuwa imewekwa kuwa mwanamke ana haki ya kupata huduma ya Afya 'inayopatikana'. Neno inayopatikana lilizua mjadala sana na kutafsiriwa kuwa lingeweza kumaanisha kuwa Haki hiyo itatekelezwa tu kama inapatikana. Katika Rasimu ya pili neno hilo limeondolewa.

Pia suala la wanawake kupata fursa na ujira sawa na mwanaume katika kazi zenye sifa zinazofanana limeongezwa.

Haki za Wazee

Katika Ibara ya 48 haki za wazee, ibara hii imeboreshwa kwa kuongeza haki ya kupata mahitaji ya msingi kutoka kwenye familia zao, jamii na mamlaka ya nchi.

> Angalizo: Katika Haki zote za makundi zilizotajwa, hakuna tafsiri za makundi hayo isipokuwa haki za makundi madogo.

Ibara ya 53 inayotoa wajibu wa Mamlaka za nchi imeweka bayana kuwa Mikataba ya kikanda na ile ya kimataifa kuhusu haki za binadamu ambayo Jamhuri ya Muungano imeridhia, [isipokuwa masharti ambayo Jamhuri ya Muungano imeeleza kutojifunga nayo] zitakuwa sehemu ya haki za binadamu zilizoainishwa katika sura ya 4 ya rasimu hii ya pili.Usimamizi wa Haki za binadamu umeainishwa katika ibara ya 54 kwa maelezo kuwa: Mahakama au chombo chochote cha kimaamuzi vinapaswa kufuata misingi ya haki ya usawa, utu na uhuru wa mtu binafsi, sheria za kimataifa za haki za binadamu na haki za jamii na maslahi ya jamii kwa ujumla wakati wa kutafsiri masharti ya sura ya nne inayohusu haki za binadamu.

Uraia wa kuzaliwa, Ibara ya 57 (5) imeongezwa ikifafanua ibara ya ndogo ya (4) iliyokua inatoa uraia wa kuzaliwa kwa mtoto ambaye wazazi wake hawafahamiki na amekutwa ndani ya Jamhuri ya Muungano Kwa mujibu wa ibara hii ndogo ya 5 endapo uraia wa wazazi wa mtoto aliyepewa uraia ukibainika si uraia wa Jamhuri ya Muungano, uraia wa mtoto huyo utasitishwa.

Uraia wa kuandikishwa, ibara ya 58 (2) imepewa ufafanuzi zaidi kuliko ilivyokuwa katika rasimu ya kwanza kwani inaeleza kuwa mtu aliyedumu kwenye ndoa yake na raia wa Jamhuri ya Muungano kwa zaidi ya miaka mitano anaweza kuomba uraia wa kuandikishwa. Endapo ndoa itavunjika na mtu huyo hakuukana uraia wake ataendelea kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano (Ibara ya 58 (3).

Hadhi ya watu wenye asili au nasaba ya Tanzania, ibara ya 59 imeongezwa katika rasimu hii ya pili kwenye sura ya 5 ikitoa ufafanuzi kuwa mtu mwenye asili au nasaba ya Tanzania ambaye ameacha kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano kwa kupata uraia wa nchi nyingine, atakapokuwa kwenye Jamhuri ya Muungano atapata hadhi kama itakavyoainishwa kwenye sheria za nchi.

DHAMIRA YA TATU: UTAWALA NA SERIKALI

Sifa za rais zimeboreshwa katika ibara ya 79 (iliyokuwa ibara ya 75 katika rasimu ya kwanza) kwa kubadili sifa ya kuwa na angalau mzazi mmoja raia wa Tanzania na kuweka kuwa wazazi wake wote wawili wawe raia wa Jamhuri ya Muungano. Pia ibara ndogo ya (h) inaongeza sifa ya kuwa awe muadilifu, anayeheshimu haki za binadamu, asiyedharau wala kubagua watu, anayefuata maadili ya viongozi na mwenendo wake hautiliwi shaka na jamii.

Kunaweza kuwa na mgombea huru – hii ilikua Ibara ya 75 (g) kwenye rasimu ya kwanza na sasa ni Ibara ya 79(f).

DHAMIRA YA NNE: BUNGE

Kupunguzwa kwa idadi ya wabunge - rasimu inapendekeza idadi ya wabunge wa bunge la Muungano kuwa 70, ambapo 50 kutoka Tanganyika na 20 kutoka Zanzibar. (Ibara ya 113).
Kila jimbo la uchaguzi litakuwa na wabunge wawili, mwanaume na mwanamke. Hii itawezesha kuwa na uwiano wa 50% kwa 50% kati ya wabunge wanawake na wabunge wanaume.

Bunge halitoweza kubadilisha masharti yaliyo kwenye sura ya I, II na IV, masharti ya ibara ya 60 na 79 hadi kwanza mabadiliko hayo yaungwe mkono na theluthi mbili ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano kutoka kila upande wa Jamhuri ya Muungano kwa kura ya maoni itakayosimamiwa na Tume huru ya uchaguzi (Ibara ya 119). Sura hizi zinahusu jina, mipaka, alama, lugha na tunu za taifa(I), Malengo muhimu, misingi ya mwelekeo wa shughuli za serikali na sera za kitaifa (II), Haki za Binadamu(IV), Muundo wa Jamhuri ya Muungano(60), na Sifa za rais (79).

DHAMIRA YA TANO: MAHAKAMA

Rasimu ya katiba katika ibara ya 153 imeainisha vyombo vya utoaji haki katika muundo wa mahakama kama ifuatavyo;

a) Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
b) Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
c) Mahakama Kuu ya Tanganyika na Mahakama kuu ya Zanzibar



UTUMISHI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

Rasimu ya katiba katika ibara ya 184 imefafanua misingi mikuu ya utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano katika vipengele vikuu kumi kati ya hivyo ni kwamba;

Utumishi wa umma ni dhamana kutoka kwa wananchi na hivyo mtumishi anatakiwa kutumikia wananchi kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu. (Ibara ya 184 (a))

Kutoa huduma kwa umma kwa njia ya haki, usawa na bila upendeleo (184(d))

Hata hivyo utumishi wa umma na uongozi katika Jamhuri ya Muungano utazingatia misingi kwamba utoaji wa ajira na uteuzi wa viongozi utakuwa kwa uwiano baina ya Washirika wa Muungano, kwa kuzingatia weledi na taaluma katika eneo au nyanja husika.

DHAMIRA YA SITA: UCHAGUZI NA VYAMA VYA SIASA

Haki ya ushiriki wa wananchi katika vyombo vya uwakilishi imefafanuliwa katika Ibara ya 189 kuwa kila raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye umri wa miaka kumi na nane au zaidi mwenye akili timamu ana haki ya kupiga kura na haki ya kuandikishwa kwa ajili ya kupiga kura katika uchaguzi au kura ya maoni.
Ibara ya 191 imetoa fursa kwa asasi za kiraia zisizokuwa za kiserikali kupendekeza majina ya watu wanaoweza kuteuliwa kuwa mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wa Tume huru ya uchaguzi.

DHAMIRA YA SABA: MUUNDO WA JAMHURI YA MUUNGANO

Muundo wa muungano ni shirikisho la serikali tatu ; serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, serikali ya mapinduzi ya Zanzibar na serikali ya Tanganyika, ibara ya 60. Rasimu hii imerudisha neno Tanganyika badala ya Tanzania bara.

Mambo ya Muungano ni 7 nayo ni; [Kama yalivyoainishwa katika jedwali namba moja]

1. Katiba na mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
2. Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
3. Uraia na Uhamiaji;
4. Sarafu na Benki Kuu;
5. Mambo ya Nje;
6. Usajili wa Vyama vya Siasa; na
7. Ushuru wa bidhaa na mapato yasiyo ya kodi yatokanayo na mambo ya Muungano.

DHAMIRA YA NANE: TAASISI ZA UWAJIBIKAJI

Rasimu imeunda taasisi mbalimbali za uwajibikaji lakini zenye maboresho ni kama ifuatavyo;

Tume ya Mahusiano na Uratibu wa Serikali (Ibara ya 109)
Tume hii itasimamia na kuratibu mahusiano baina ya Serikali ya Muungano na Serikali za Washirika wa Muungano na kusimamia na kuratibu mahusiano

baina ya Serikali za Washirika wa Muungano. Majukumu ya tume hii kama yalivyoainishwa katika ibara ya 111 ya rasimu ni kuwezesha uratibu na ushirikiano katika kutekeleza masharti ya katiba hii, sera, sheria, mipango na mikakati baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za washirika wa Muungano na baina ya Serikali za Washirika.

Tume ya Utumishi ya Umma (Ibara ya 186) Hiki ni chombo cha juu katika utumishi wa umma chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote kuhusu utumishi wa umma. Ibara ya 186 (3) imeongeza sifa za mwenyekiti na wajumbe wa tume kuwa awe na upeo mkubwa katika mambo ya utumishi, utawala na jamii katika kipindi kisichopungua miaka kumi.

Tume Huru ya Uchaguzi

Tume hii imeundwa kwa ajili ya kusimamia na kuratibu shughuli za uchaguzi na masuala yanayohusu vyama vya siasa. Ibara ya 194 (2) (iliyokua ibara ya 185 katika rasimu ya kwanza) inayohusu Malalamiko kuhusu uchaguzi, imeboreshwa kwa kueleza kuwa kesi za malalamiko kuhusu uchaguzi wa wabunge zitafunguliwa mahakama kuu mara tu matokeo yatakapotangazwa na si katika mahakama ya Rufaa kama ilivyokua katika rasimu ya kwanza.

Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji

Rasimu hii imeboreshwa zaidi kwa kuongeza ibara ya 201 inayohusu uteuzi na sifa za wajumbe wa Tume. Pia ibara ya 202 inayohusu kamati maalum ya uteuzi nayo imeongezwa. Wajumbe wa Tume watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na kamati maalum ya uteuzi (Ibara ya (200:2).

Vilevile katika ibara ya 208 imeundwa Tume ya Haki za Binadamu, ambayo itakuwa na Mwenyekiti, Makamu mwenyekiti na Wajumbe wasiozidi saba watakaoteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na kamati maalum ya uteuzi. Pia majukumu ya Tume hii kama yalivyo katika ibara ya 210 ya rasimu yameongezwa ikiwa ni pamoja na kuihamasisha serikali kutia saini na kuridhia mikataba au makubaliano ya kimataifa yanayohusu haki za binadamu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Ibara ya 219 imeboresha iliyokua ibara 204 katika rasimu ya kwanza kwa kuongeza vifungu vinavyohusu taratibu za kuondolewa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali endapo atakuwa amekiuka kanuni za maadili na miiko ya uongozi wa umma (Ibara ya 219(3) na (4).

HITIMISHO

Pamoja na maboresho yaliyofanyika katika Rasimu, vilevile bado yapo mapungufu kadhaa tunayofikiri yanayohitaji yafanyiwe marekebisho na Bunge Maalum la Katiba ili kupata katiba iliyo bora zaidi.

1. Haki ya kuishi bado ni kwa mujibu wa sheria, kifungu hiki kinaonyesha kuwa haki hii bado inaweza kuminywa na sheria na hivyo kuwepo uendelezwaji wa adhabu ya kifo ambayo inakiuka haki ya kuishi, Ibara ya 24
2. Rais ana mamlaka ya kuidhinisha utekelezaji wa adhabu ya kifo iliyotolewa kwa mujibu wa sheria, Ibara ya 72 (1) k.
3. Ibara ya 24, 31 na 33 haki hizi zimefungwa na maneno kwa "mujibu wa sheria" au "kwa kuzingatia sheria" hivyo hii inatoa upenyo kutungwa sheria ambazo zitaondoa kabisa haki hizi.

4. Rasimu haijatoa mwongozo wa kina kuhusu rasilimali muhimu kwa nchi wanachama wa Jamhuri ya Muungano, kwa mfano rasimu imegusa kwa kiasi kidogo sana masuala ya ardhi Ibara ya 7(2) d.

5. Rasimu imeweka nafasi za Majaji wakuu watatu (Jaji Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Jaji Mkuu wa Tanzania Bara na Jaji Mkuu wa Zanzibar) Pendekezo letu ni kuwa kuwe na Jaji Mkuu mmoja tu na huyo ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Majaji wengine wawili waende kwa cheo cha Jaji Kiongozi ambaye kwa sasa cheo hicho hakiko kwenye katiba. Kuanzia Sura yote ya 10.

6. Rasimu haikueleza kuhusu lugha ya mahakama. Pendekezo; Lugha ya mahakama iwe ni Kiswahili na kuhakikisha kuwa sheria zote za nchi zinaandaliwa kwa lugha ya Kiswahili.

7. Rasimu ipo kimya kuhusu masuala ya ushirikiano wa kikanda kwa mfano Jumuiya ya Afrika Mashariki

8. Rasimu haijatoa mwongozo kuhusu madeni ya serikali na jinsi gani ya kuzuia serikali kukopa sana na kuongeza deni la taifa

9. Rasimu imezungumzia tu uwajibishwaji wa viongozi wa umma lakini ipo kimya kuhusu maadili katika jamii na jinsi ya kuwawajibisha wananchi wanaochangia katika mmomonyoko wa maadili katika jamii.

10. Bado kuna mapungufu katika haki za kijamii. Ingekuwa ni vyema iwapo kungekuwa na ibara inayozungumzia haki ya kuanzisha na kuwa na familia. Hii itatoa umri ambao mtu anaweza kuoa au kuolewa ili mtu yeyote asiolewe kabla hajatimiza umri wa miaka 18 na pia suala la ndoa liwe ni la hiari na lisihusishwe ridhaa za mahakama au ridhaa ya wazazi. Pia kuwe na mahakama za familia.

11. Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa haipo kabisa katika rasimu hii ya pili, ni muhimu kwa chombo hiki kuwa cha kikatiba. (Haijatajwa).

12. Katika Taasisi za Uwajibikaji inapendekezwa iongezwe Taasisi ya kusimamia utendaji wa Jeshi la polisi ukizingatia kumekua na utendaji usioridhisha sana wa jinsi Baadhi ya polisi wanavyotekeleza majukumu yao kinyume na sheria na taratibu za kazi yao.

13. Haki ya Afya haijatajwa katika Rasimu, tunapendekeza haki hii muhimu iwepo katika katiba

Justice Lugakingira House,Kijitonyama
S.L.P 75254, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2773038/48
Tovuti:www.humanrights.or.tz

policy forum

Kitalu 14, Barabara ya Sembeti, Kandoni mwa
Barabara ya Bagamoyo ya zamani, Mikocheni B,
S.L.P 38486, Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2780200/782317434
Tovuti: www.policyforum.or.tz